# MWONGOZO WA MSHALE WA MATUMAINI GREDI SABA

NOVELA

APRIL 26, 2024
BW. BRIAN AMUKOYA MAFU
YOUTUBE BW. BRIAN AMUKOYA MAFU/0745171371

# MWONGOZO WA NOVELA MSHALE WA MATUMAINI GREDI SABA

Novela ni utungo wa kifasihi unaoandikwa kwa lugha ya kimjazo au kinathari.

Kimeandikwa na profesa John Habwe na kupigwa chapwa na Access Publisher Limited.

Kina jumla ya sura kumi.

Profesa John Habwe ni mhadhari wa Kiswahili katika chuo kikuu cha Nairobi.

Habwe ni mwandishi wa hadithi aliye na uzoefu mkubwa sana .

## PLOTI.

Zingo na mamake Zahara wanakimbilia ughaibuni Gera katika Jamhuri ya Demokrasia ya Tereka kufuatia mzozo wa kikabila kati ya Walanga na Wareba katika nchi yao ya Doneka.Huko ughaibuni wanakabiliana na matatizo mengi .Zingo anafanya bidii kuyakabili licha ya umri wake mdogo.Hata hivyo, kinachomstaajabisha na kumhuzunisha

ni kuhusishwa na baba yake Kadurenge ambaye anatuhumiwa kuwa mhalifu wa kivita .Zingo anabaguliwa na wenzake lakini anapiga moyo konde na kuendelea na masomo yake ambayo sasa yanampa matumaini ya kuyageuza maisha yake ya karaha kuwa ya furaha baada ya kifo cha mamake.

Hii ni hadithi ya huzuni inayofunua makovu ya mizozo ya kijamii hasa mizozo hiyo inavyoathiri vijana wadogo.

**Sifa za Novela**

1. Maandishi ya kinathari :- Kinachosimuliwa huwasilishwa kwa maelezo marefu yanayogawanywa katika aya na hata sura maalum.
2. Ufupi :- Kiumbo , novela ni fupi na inaweza kusomwa kwa kikao kimoja tu; hata hivyo, ina urefu unaoruhusu kujengeka kwa msuko na wahusika wanaokuza hadithi maalum.
3. Usahihi wa muundo :- Novela ina muundo sahihi na mwepesi .Si changamano kama riwaya.

**WAHUSIKA KATIKA FASIHI ANDISHI.**

Fasihi andishi hutumia wahusika wanadamu ,kinyume na fasihi simulizi ambayo hutumia wahusika changamano.

**Aina ya wahusika**

A. Wahusika Wakuu :- Huwa ni wahusika ambao wanahusishwa na takribani visa vyote katika novela.
Huhusishwa kutoka mwanzo hadi mwisho .Aghalabu mhusika mkuu hafi isipokuwa hufa kifo cha ushujaa.

B. Wahusika wasaidizi :- Ni wale wanaosaidia kujenga mhusika mkuu.
Hutokeza mara nyingi katika hadithi.

C. Wahusika wadogo :- Hawa hufanya kazi ndogo sana katika fasihi kama vile kujenga maudhui au mandhari.Hawa wakitolewa .Novela inaweza kuendelea bila kubadilika sana.

D. Wahusika bapa :- Ni wahusika wasiobadilika katika mwanzo hadi mwisho.Mfano ;mhusika mbaya anabakia kuwa mbaya kutoka mwanzo hadi mwisho.

**Umuhimu wa mandhari katika Novela.**

Mandhari ni sehemu ambayo matukio ya hadithi au masimulizi hutokea .

Huweza kuwa halisi kama vile baharini,njiani, kijijini,mijini au pahali popote .

I. Hukuza maudhui mbalimbali katika novela.
II. Huonyesha jamii ambayo hadithi inasimuliwa.
III. Huendeleza ploti ya hadithi.
IV. Huonyesha nafasi ya watu fulani katika jamii.
V. Huonyesha changamoto zinazoikumba jamii fulani.
VI. Hujenga sifa za wahusika
VII. Huonyesha mahali ambapo hadithi inatokea.

## UFAAFU WA ANWANI YA MSHALE WA MATUMAINI

Anwani ya Mshale wa Matumaini imetumika kwa maana mbalimbali katika novela hii.

- Inarejelea matumaini waliokuwa nayo wakimbizi (uk 14)msimulizi anasema kuwa mshale wa matumaini ulikuwa umewafuma wote.
- Inarejelea anwani ya kitabu alichokuwa akikisoma Zingo. Kitabu hiki kilikuwa chanzo cha kujiamini kwake Zingo.
- Inarejelea wahusika waliochorwa kama nguzo ya matumaini kwa wengine ,mfano ni Mzee Musambale.
- Wanakijiji cha Mokowe ni Mshale wa Matumaini kwa wakimbizi walipokuwa wamelemewa na uchovu na njaa wanawasaidia kwa chakula na malazi.

- Inarejelea matumaini ambayo Zingo alikuwa nayo ya kurudi nyumbani kwao Doneka siku moja.
- Inarejelea fursa ambayo Zingo anapata kwenda kusomea Uswizi.
- Inarejelea matumaini ya wakimbizi wanakokwenda uhamishoni watapata fursa ya kukaa kwa amani na upendo .
- Inarejelea matumaini Zahara anayo kwamba kila jambo litakwnda sawa hadi wavamizi wanapofika kumvamia.
- Inarejelea matumaini aliyo nayo Mzee Musambale ya kupata familia yake,matumaini ambayo yanazimmwa hapo baadaye.

# MUHTASARI.

## SURA YA KWANZA

Sura ya kwanza ndiyo utangulizi wa novela hii.Katika surah ii, tunakumbushwa mhusika mkuu Zingo na wazazi wake Kadurenge Mlawatu na Bi Zahara .Sura hii inasimulia kuhusu mnongono uliokuwa unazuka hapo awali mjini Kisamale na kisha ukafifia .Huu ulikuwa uvumi wa uvamizi wa kikabila uliokuwa umepangwa na Walanga dhidi ya Wareba.Baba yake Zingo alikuwa mlanga hali mama yake alikuwa mreba.Mama yake Zingo hakuamini hata kidogo ukweli wa mnongono huo

lakini baba yake alionekana na kuwa na uhakika kuhusu uvamizi uliopangwa.Kadurenge alikuwa na chuki dhidi ya Wareba kwa vile aliamini kuwa walikuwa wakipendelewa uongozini ,kazini na hata katika biashara.Katika sura hii tunajulishwa kuwa Zahara alikuwa mfanyabiashara pale mjini na Kadurenge alikuwa mwalimu wa shule ya msingi.Zingo mwana wao alikuwa mwanafunzi.

**ZOEZI**

1. Matukio katika sura hii yanafanyika wapi?
2. Wahusika waliotajwa wana uhusiano gani? Jadili..
3. Unajifunnza mambo gani kutokana na sura hii?
4. Wahusika waliotajwa katika sura hii wana sifa gani?

## SURA YA PILI

Katika sura hii, Zingo anasimulia kuhusu usuli wake.Tunatambua kuwa alizaliwa na kukulia mjini Kisamale.Hakuwa ameshuhudia uhasama wowote wa kikabila tangu utotoni .Watu wote walitangamana na kuishi kwa amani.

Uvumi uliokuwa umesambaa kuhusu uvamizi wa Walanga ulitulia na hali ya kawaida ikarejea.Zingo

alifurahia hali hii kwani hakutaka kupoteza marafiki zake aliokuwa akicheza na kusoma nao pamoja.

Baada ya muda fulani uvumi huo ulirejea tena kwa kishindo.Watu waliingiwa na woga mwingi .Kadurenge alipendekeza familia yake kuhamia nchi jirani ya Azania au Jamhuri ya Demokrasia ya Tereka .Baada ya muda mfupi,Kadurenge alitoweka nyumbani kabisa.

Siku chache baada ya Kadurenge kutoweka vita vya kikabila vilizuka na kusababisha umwagikaji wa damu.Watu wengi walipoteza maisha na wengi kujeruhiwa .Kulikuwa na uharibifu mkubwa wa mali,watu wengi walilazimika kutoroka makwao.Zingo na mama yake walijiunga na wakimbizi wengine kuelekea Jamhuri ya Demokrasia ya Tereka , eneo la mpakani Gera.

## SURA YA TATU

Katika sura hii, Zingo pamoja na wakimbizi wengine wapo safarini kuelekea Gera.Eneo hili la Gera ambapo wakimbizi walitorekea ilikuwa ni umbali wa kilomita mia mbili.Ilikuwa siku mbili kufika hapo .Hii ilikuwa safari ngumu yenye changamotosi haba.Njiani walinyeshewa na kukosa chakula na maji.

Usiku ulipowapata safarini, mzee Musambale alipendekeza watafute mahali pa kulala kwa usalama wao.Walitafuta makao katika kijij cha Mokowe .Kijiji hiki

kilikuwa cha wakulima .Baada ya majadiliano walikubaliana kulala pale usiku huo.Aidhaa,walisaidiwa kwa kupewa chakula.

## SURA YA NNE

Sura ya nne inaendeleza matukio ya usiku kijijini Mokowe .Usiku huo wakimbizi walihisi uchovu mwingi sana kutokana na kutembea mwendo mrefu.Zingo aliona heri akisome kitabu alichokibeba cha Mshale wa Matumaini ili kujiongezea matumaini.

Baadaye chakula kiliiva ,akala na kulala.Aliota .Ndotoni alikuwa akiichezea soka timu yake ya Nomads iliyokuwa ikishindana na Ngorongoro .Ingawa alifanikiwa kuifungia timu yake magoli mawili.Wapinzani wao waliyakomboa na kuwashinda.Timu yake ilimshambulia refa alipokataa kuwaongezea muda wa ziada .Jambo lililowafanya wenzao kuingilia fujo hiyo.

Alikimbizwa na mchezaji aliyeshika gongo mkononi.Juhudi za kumrai amsamehe ziliambulia patupu.Akiwa karibu kumpasua kichwa,Zingo alipiga unyende mkubwa sana.Hapo ndipo alipogutuka na akabaini kuwa ilikuwa ni ndoto tu.

Safari ya kuelekea Gera ilirejelewa asubuhi na mapema.Mzee Musambale aliongoza kikundi cha watu wasiopungua ishirini.Aliwahimiza wasife moyo kwani walikuwa karibu kufika mpakani.Njiani walimpoteza Bi.

Zulu aliyelemewa na mwendo wa masafa marefu.Kifo chake kilimhuzunisha Zingo na wenzake sana.Baada ya kuulaza mwili wake kichakani ,waliendelea na safari.Hatimaye walifanikiwa kufika Gera mwendo wa saa kumi jioni.Baadhi ya kusajiliwa kama wakimbizi ,walikabidhiwa mahema yao ili kuanza maisha yao pale kambini.

## SURA YA TANO

Sura hii inatangulia ukurasa wa maisha mapya ya wakimbizi kambini.Maisha haya yalikuwa tofauti na maisha waliokuwa wameyazoea .Mchana jua lilichoma Zaidi na usiku baridi kali .Kule kambini wakimbizi waliishi kwa hofu ya kuingiliwa na wezi na wabakaji.

Maisha mapya ya kambini yaliweza kuwaathiri watu kwa njia tofauti .Zahara ni mmoja kati ya walioathirika sana.Alipatwa na msongo wa mawazo na kuathiri afya yake.Afya yake ilidorora na kumfanya mnyonge .Zingo alidhania kuwa mama yake aliathiriwa na mabadiliko ya maisha yao.

Zahara alimsajili Zingo katika shule ya upili ya Gera Secondary for Refugee Children kidato cha kwanza. Siku moja Zingo alikutana na rafiki yake Deno pale kambini .Alistaajabu kumwona Deno akilia sana alipomuuliza habari za wazazi wake.Kisha akakimbia na kumwacha .Hata hivyo, bahati iliwakutanisha tena siku nyingine

.Hapo ndipo Deno alipomjulisha kwamba alishuhudia Kadurenge akichoma nyumba yao na kuwateketeza wazazi wake.

Siku moja Zingo alimkaribisha Deno katika hema lao.Hata hivyo,maombi yake yalikuwa kwamba mama yake asingemuuliza Deno habari za wazazi wake.Angefanya hivyo,ukatili wa baba yake ungefichuka.

## SURA YA SITA

Urafiki wa Zingo na Deno ulizidi kuimarika kila siku.Zingo alimshauri Deno ahamie katika hema lao.Mama yake hakuwa na pingamizi hata kidogo.Siku zilisonga na mama yake hakuonyesha ahueni.Ilibidi Deno na Zingo kumsaidia kutekeleza majukumu ya pale nyumbani.Tayari walikuwa wamepewa kijisehemu cha shamba walipojenga nyumba yao ya udongo.Deno alikataa ushauri wa Mzee Musambale kumtaka ajiunge na shule.

Siku moja Musambale aliwatembelea na kumjulisha Zahara habari za mumewe Kadurenge. Aliwajulisha kwamba redio ilikuwa imetangaza kwamba Kadurenge na wengine walikamatwa na jeshi la Umoja wa Mataifa huko Doneka. Walishukiwa kushiriki katika mauaji ya halaiki ya watu.Habari hizi ziliwakosesha raha wote waliokuwapo .Zahara aliathirika sana na habari hizo na kumfanya kulazwa hospitalini siku

zilizofuata.Ugonjwa wa shinikizo la damu ulikuwa umezidi maradufu , kwa bahati mbaya hali yake ilikosa kuimarika na mwishowe akafariki.

## ZOEZI

1. Taja wahusika katika sura hii?
2. Wahusika uliowataja wana uhusiano gani ?
3. Wahusika hao wana sifa gani?
4. Taja maudhui yanayojitokeza katika sura hii ?
5. Taja mandhari yanayojitokeza katika sura hii ?

# SURA YA SABA

Kifo cha Zahara kilimgusa sana Zingo .Siku nyingi alishinda akimwaza mama yake .Alitamani pia kukutana na baba yake.Alijuta kuzaliwa katika nchi ya Doneka iliyokuwa na misukosuko mingi katika kitabu cha Mshale Wa Matumaini .Hapo alipata kufahamu kuwa maisha yana pandashuka nyingi na ni muhimu mtu kujithamini kwa hali zote.Rafikiye wa karibu Deno mara kwa mara alimshauri asikate tamaa.Hakuwa na matumaini ya kuendelea na masomo lakini Mzee Musambale alimsihi aendelee .Shuleni alikuwa na matumaini ya kufanya vyema ili apate ufadhili wa masomo kule Uswizi.

Jumapili moja walipanga kumjulia hali Mzee Musambale kwake .Baada ya mazungumzo ya muda waliamua kusikiliza matangazo ya redio.Ilikuwa idhaa ya BBC

habari za Afrika.Jioni hiyo habari zilizogonga vichwa vya habari zilihusu kushikwa kwa magaidi sugu nchini Doneka .Jina la Kadurenge Mlawatu lilitajwa miongoni mwa magaidi hao.Habari hizi ziliathiri uhusiano kati ya Zingo na wenzake ,Mzee Musambale na Deno.

**ZOEZI**

1. Eleza matukio makuu katika sura hii ?
2. Eleza jinsi matukio hayo yanawaathiri wahusika katika sura hii ?

## SURA YA NANE

Sura hii inasimulia Zingo anavyobaguliwa na wenzake kwa ajili ya vitendo vya baba yake. Mchezoni na masomoni alianza kutengwa na wenzake na hata walimu.Alitamani kurudi nyumbani Doneka.Rafiki yake Deno naye alibadilika kitabia na kuingilia utumiaji wa mihadarati .Hakupatikana nyumbani mara nyingi.Mara kwa mara Zingo aliwaza kuacha shule lakini hakuwa na pa kwenda.Aliamua kupata ushauri kutoka kwa idara za shule,jambo lililompatia matumaini masomoni.

Isitoshe ,alimkumbuka Mungu wake na kumwomba kila alipopatana na changamoto zozote.Jumapili alihudhuria ibada ijapokuwa alipitia unyanyapaa

kutoka kwa baadhi ya waumini .Usiku mmoja aliota akienda Uswizi kwa masomo ya juu.

**ZOEZI**

1. Eleza sifa moja ya Zingo inayojitokeza katika sura hii?
2. Taja maudhui yanayojitokeza katika sura hii ?
3. Ni mandhari gani yaliyotumiwa katika sura hii ?

## SURA YA TISA

Maisha ya Gera yalizidi kuwa magumu kila siku japokuwa Zingo aliishi nyumba moja na Deno,urafiki wao ulikuwa umeanza kusambaratika kwa sababu ya upweke ,Zingo alimwaza mama yake mara kwa mara .Mzee Musambale hakuwacha kumpa ushauri wake.Habari za vita huko Doneka ziliendelea kupokelewa kila siku.Vita hivyo havikuwa rahisi kuvizima.Maelfu walikuwa wamepoteza maisha na wengine kuwa wakimbizi .Tabia ya Deno ilikuwa imebadilika sana na kuanza kumiliki vitu vya bei ghali kama vile simu na saa.Siku moja aliamua kufunganya virago vyake na kuondoka nyumbani walipokuwa wakiishi. Hali ya afya ya Mzee Musambale ilikuwa imeanza kudorora .Aliathirika sana kutambua kuwa Kadurenge alichangia .

SIku moja Zingo alipanga kumtembelea ili kumjulia hali.Hali yake haikutamanisha tena.Kuna siku moja

walipokea uvumi kwamba Mlima Gera ungelipuka tena baada ya miaka kumi.Uvumi huo ulijaza hofu na wasiwasi miongoni mwa wakimbizi .Shirika la Canada lililoshughulikia wakimbizi lilijitolea kuwahamisha wakimbizi eneo salama .Watu walikataa pendekezo hilo.Baadaye habari hizo ziligunduliwa kuwa tetesi zisizokuwa na msingi.

Zingo alikuwa na matumaini ya juu masomoni.Alitamani kusomea uanasheria ili kutetea haki za watoto huko Doneka .Deno alikamatwa miongoni mwa vijana sitini walioshitakiwa kwa wizi na ubakaji pale kambini.

# SURA YA KUMI

Katika sura hii matokeo ya kidato cha nne yalitoka.Katika shule walikosomea wakimbizi pekee Zingo aliibuka kuwa mwanafunzi bora Zaidi.Azma yake ya kwenda kusomea taaluma ya sheria nchini Uswizi ilirejea kwa kishindo.Matamanio yake baada ya kusoma yalikuwa kurejea Doneka ili kupatanisha makabila ya Walanga na Wareba japo Mzee Musambale alikuwa amezidiwa na maradhi,ufanisi wa Zingo ulimfurahisha sana.Hata hivyo,baada ya siku chache ripoti za kifo chake zilipokelewa.Habari hizi zilimsikitisha Zingo sana.Mazishi ya Mzee Musambale yalihudhuriwa na watu wengi wa matabaka mbalimbali.Alisifiwa na

wazungumzaji kwa hisani na ujasiri wake.Kila mnenaji alitaka amani iwekwe na wakimbizi warudishwe nyumbani.Kwa woga Zingo alisimama na kusema yaliyokuwa yakimpita moyoni.Alitaka Watoto wasihusishwe kwa ugomvi wa watu wazima.Watoto walikuwa wameadhiriwa sana na mapigano hayo.Kufa kwa Mzee Musambale kulimwacha na hofu nyingi.Hakujua ni nani atamfuata Mzee Musambale.

Nafasi ya Zingo ya kusomea Uswizi iliwadia na akaletewa fomu ajaze.Alipangiwa kusafiri baada ya miezi sita.Hatimaye siku ya kwenda ilifika na akaikumbuka ndoto yake ya awali.Akiwa safarini alikisoma kitabu chake cha Mshale wa Matumaini hadi ukurasa wa mwisho.Alifurahia kifungu cha mwisho kilichoeleza kuwa " pindi jambo likiisha kuamuluwa basi jambo hilo linawezekana ",Azma yake ya kusomea Uswizi ilikuwa afaulu ili arudi Doneka kutetea haki za wanyonge hasa watoto.

# MAUDHUI KATIKA NOVELA

Maudhui ni mambo muhimu yanayoelezwa katika hadithi,riaya ,novela ,hotuba au nakala.

## 1. Maudhui ya Elimu

Mfumo wa mafunzo yanayopatikana shuleni,vyuoni au maishani.

Pia ni taaluma au masomo.

- Kadurenge alikuwa mwalimu katika shule ya msingi ya Nakitare. (uk 2)
- Zingo alikuwa akidurusu somo la Kifaransa wakati (uk 4)
- Zingo anapekuapekua kurasa chache za kitabu cha Mshale wa Matumaini…(uk 10)
- Zingo anaingizwa shuleni pale kambini na mamake,anajiunga na kidato cha kwanza..( uk 25)
- Masomo yalikuwa na changamoto nyingi pale shuleni ….(uk 26)
- Deno hakutaka kujiunga ba shule yoyote …….(uk 30)
- Zingo alichuana na vitabu bila kuchoka…(uk 51)
- Zingo alikuwa akiomba ushauri kutoka kwa idara mbalimbali za shule…(uk 43)
- Zingo anaamua kurejea shuleni baada ya kuuwazia ushauri wa Mzee Musambale..(uk 37)
- Zingo anatokea kuwa kidedea katika shule yao katika mtihani wa kitaifa wa kidato cha nne…(uk 56)

## 2. Maudhui ya ukatili.

Ukatili ni hali ya kukosa kuwa na huruma; udhalimu,uovu.

- Watu walipigana damu zikamwagika kama maji,watu wengi walikufa…..(uk 8-9)
- Miili ya wafu ilikuwa imepatakaa ungedhani ni walikuwa kuku……(uk 12)
- Sauti za bunduki zilisikika zikialika hapa na pale…..(uk 12)
- “Babake Zingo aliteketeza nyumba yao Deno na kuwaunguza wazazi wake…..(uk 27,,29)
- Kadurenge pamoja na wengine walihusika katika ukatili na unyama….(uk 31-32)
- Wote waliopanga uvamizi na uteketaji wa makanisa na maboma ya watu walishikwa…(uk 39)
- Kambi za wakimbizi zililalamikia unajisi, wizi na uchawi…(uk 52)

## 3. Maudhui ya dini.

Dini ni Imani inayohusiana na kuwapo kwa Mungu au miungu.

- Zingo alikumbuka hadithi aliyofundishwa na mwalimu wa somo la Dini …..(uk 13-14)
- Zingo aliyapenda mafunzo ya Yufusu,Danieli na Daudi kwenye Biblia…..(uk 25)
- Zingo anajifunza kuomba mungu Zaidi,kila jumapili alienda kanisani…..(uk 44)
- Zingo aliomba Mungu azidi kumfundisha na kumuelekeza jinsi ya kuchagua maisha mema….(uk 45)

**Tanabahi** : Maudhui mengine katika novela ni Mabadiliko,

Ndoa, Malezi n.k.

## MBINU ZA LUGHA / UANDISHI KATIKA NOVELA.

### A. Tashbihi.

Tashbihi ni tamathali ya usanifu ya kufananisha vitu kulingana na hali au mienendo yao.

- Alitulia tuli kama maji ya bwawani….(uk 5)
- Huu ni kama mtengo wa panya ushikao waliomo na wasiokuwemo… (uk 5)
- …..damu zikamwagika kama maji….(uk 8)
- Sauti ya mama ililipuka kama fataki…(uk 10)
- Nilitoka kama mwizi…..(uk 11)
- Akajinyoosha twaa kama sanamu ya kuchonga…(uk 22)
- ….tupwa kama mbwa….(uk 22)
- …nilikuwa kama mgomba ……(uk 35)
- …ule mithili ya mfiwa….(uk 41)
- …alikonda kama ng'onda….(uk 24)
- …nilivizamia kama mchwa katika ujenzi …..(uk 52)
- …nyumbani huko nilikuona kama msitu wa simba….(uk 17)

### B. Semi/ Nahau

Nahau ni kifungu cha maneno yenye maana maalum isiyotokana na maana za kawaida za maneno hayo.

- ❖ Watu waliopiga soga….(uk 1)
- ❖ …..swala la kikabila nchini mwetu lilikuwa donda sugu…..(uk 2)
- ❖ …….lazima kutawaka moto…(uk 5)
- ❖ …mambo hayangetumbukia nyongo kama yalivyotokea..(uk 8,,28)
- ❖ ….tulikuwa tumekata shauri kutorokea mahali popote…(uk 9)
- ❖ ….Nilipiga moyo konde ……(uk 17,,45)
- ❖ …Kila mtu alishika roho yake mkononi….(uk 12)
- ❖ Mimi na mama yangu tuliponea kwa tundu la sindano….(uk 9)

## C.Methali.

Usemi unaoaminiwa kuwa na ukweli wenye maana iliyofumbwa isiyoelezeka kwa maneno yaliyotumika.

- Chendacho mavani hakina marejeo….(uk 22)
  Mavani : makaburi; maziarani.
  Kitu kiendacho kuzikwa kaburini hakiwezi kuwepo tena.
  - Mkono wa kifo kwa kweli hauna kilio..(uk 23)
  - Maji yakimwagika hayazoleki…(uk 36)

Maji yaliyomwagika tayari hayawezi kuokotwa tena,,ni sawa na methali : la kuvunda halina ubani..sikio la kufa halisikii dawa.

- Mtoto wa nyoka ni nyoka….(uk 42)
  Kinachozaliwa na nyoka lazima kiwe ni nyoka vile vile
  Mtoto hufuata tabia na maumbile ya mzazi wake.
  - Kuinamako ndiko kuinukako….(uk 44)
    Mahali kwenye mabonde kunaweza kubadilika na kuwa na mwinuko
    Watu maskini pia wanaweza kujaliwa na kupata uwezo kwa hivyo tusiwadharau kwa njia yoyote.

## D. Tashihisi /Uhaishaji

Ni usemaji wa lugha ambao hukifanya kitu kisicho na uhai kupewa sifa ya kitu chenye uhai.

- Mnongono ulikita mizizi na kuendelea kusambaa……
- Mnongono ulizidi kuvuma……
- Uvumi ulibisha hodi….(uk 7)
- …..sauti ya mama ilipasua hewa kama radi ya mvua ya kidindia …(uk 11)
- Macho yake yalinikemea…(uk 13)
- Upepo uliovuma kwa hasira kubwa sana …(uk 17)

- Ungesikia miguu yao ilivyoumana na barabara …(uk 21)
- …kilinidunga mwiba mchungu kifuani…(uk 22)
- …..ilikuwa inapambana na mawingu angani…(uk 45)
- Ndege ilikuwa inavuka bahari ya Atlantiki
- Mkono wa serikali haukufa moyo…..(uk 52)
- …yangekunoa ukapata makali….(uk 53)
- Maisha ya Bi. Zulu yalimzika ghafla …(uk 23)
- Ugumu wa maisha haya ulikuwa mwalimu tosha…..(uk 53)

## SIFA ZA WAHUSIKA KATIKA NOVELA.

### A. ZINGO

- ✔ Ni mhusika mkuu katika novela mshale wa matumaini.
- ✔ Ni mwanawe Zahara na Kadurenge Mlawatu.
- ✔ Mwanafunzi katika shule ya msingi ya Nakitare na pale kambini shule ya upili ya Gera katika kidato cha kwanza.

❖ **Mwenye Bidii** :- anatia bidii masomoni ..
Anashughulikia kazi za nyumbani wakati
Mamake anaugua.
Anachapua miguu kukaza mwendo l

licha ya kuwa mchovu sana.

- **Jasiri** :- Anasimama mbele ya waombolezaji katika mazishi ya Mzee Musambale.
- **Msomi** :- Muda mwingi alikuwa akisoma novela yake .
  Alichuana na vitabu bila kuchoka.
  Alifaulu katika mtihani wa taifa kuliko mwanafunzi mwingine yeyote.
- **Mcha Mungu** :- Kila jumapili alienda kanisani kuomba Mungu.
  Alimshukuru Mola wake kwa neema baada ya taarifa kwamba watahamishiwa sehemu salama.
- **Mpenda Amani** :- Hakutaka mzozo baina yake na wenzake pale shuleni ….
  Alifurahia kuona amani ilirejea na watu waliendelea na shughuli zao .
- **Mzalendo** :- anahamu ya kurudi nyumbani kwao Doneka licha ya vita kuendelea huko..

## B. KADURENGE MLAWATU

- ✔ Mumewe Zahara na babaye Zingo.
- ✔ Mwalimu katika shule ya msingi ya Nakitare nchini Doneka.
- ✔ Ni mhusika bapa katika novela.

- ✔ Kiongozi wa kikundi cha magaidi wa kivita vya kikabila nchini Doneka.
  - ❖ **Katili** :- Alishukiwa kuhusika katika mauaji ya halaiki ya watu.
  - ❖ **Msaliti** :- alionekana akiunga mkono mzozo uliovumishwa . Aliamini kwamba kabila lake lilikandamizwa.

## C.MZEE MUSAMBALE

- ✔ Kiongozi wa kundi la wakimbizi …
- ✔ Rafiki wa karibu wa Zahara na Zingo.
- ✔ Ni mhusika msaidizi katika novela.

- ❖ **Mshauri** :- Anampa ushauri Zingo kuhusu suala la kuacha shule.
- ❖ **Mzalendo** : Alipenda kuhadithia mambo ya kale na historia nzima ya Doneka. Alipenda kusikiliza habari na muziki wa kidoneka.
- ❖ **Mcha Mungu** :-Zingo na Deno wanapomtembelea nyumbani siku ya jumapili,walimpata akiwa ametoka kanisani.

## D. BI. ZAHARA

- ✔ Mamaye Zingo na mkewe Kadurenge.
- ✔ Mfanyabiashara katika soko la Namuyange.

- ✔Mkimbizi wa vita vya kikabila nchini mwao Doneka.
- ✔Ni mhusika msaidizi katika novela.

❖ **Jasiri** :- Anaonyesha ujasiri kwa kumuuliza mumewe
ushahidi wa kutosha kudhibitisha kauli yake.

❖ **Mshauri** :- Anampa mumuwe ushauri wa kwenda mahakamani kutafuta haki….
Anampa Zingo ushauri kwamba ajikaze ,
maisha si rahisi….

❖ Mwenye Busara :-Kupitia kauli yake Zingo,anasema kuwa alimwona mamake kuwa na busara
nyingi na kuwa mtu wa kujiamini sana.
Wanawake wengine walimsikia na kumwona ,hata baadhi ya wanaume.